





Khalai ni msichana mwenye  
umri wa miaka saba. Katika  
jamii yake, jina lake lina  
maana sawa na 'aliye  
mzuri'.




Khalai anapoamka,  
anauzungumzia mmea  
mchanga wa Mchungwa  
akisema, "Tafadhali  
mchungwa, kua mkubwa  
uzae machungwa mengi  
mabivu."



Khalai anapokuwa njani  
kwenda shulen,  
anazzungumzia Nyasi.  
Anasema, "Tafadhal nyasi,  
zidi kuwa kijani kibichi na  
wala usinyauke."



Khalai anapoyapita Maua ya  
kichakani, anasema,  
"Tafadhal maua, endelea  
kunawiri ili nikutumie  
kuzirembesha nywele  
zangu."



Anapokuwa shuleni, Khalai anauzungumzia Mti ulioko pale shuleni, "Tafadhalii miti, yazaee matawi makubwa ili tuweze kusomea chini ya kivuli chako."



Khalai anauzungumzia ua  
unaoizingira shule yake,  
"Tafadhalu ua, kua uwe  
mwenye nguvu ili uilinde  
shule yetu dhidi ya watu  
wabaya."



Anaporudi nyumbani alasiri,  
Khalai anautelelea mti wa  
mchungwa kutazama ikiwa  
machungwa yameiva.



"Machungwa bado mabichi,"  
Khalai anashusha pumzi.  
"Nitakutembelea kesho,  
mchungwa wee! Labda  
utanipa chungwa mbivu  
wakati huo."